**Makala**
40300 | Januari 2017

**Luc Christiaensen, Joachim De Weerdt, & Ravi Kanbur**

International Growth Centre

# Mchango wa Miji Midogo

## Katika Kuleta Maendeleo na Kuondoa Umaskini Tanzania



**Kwa Kifupi**

- Miji ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi. Nchini Tanzania miji inakua kwa kasi. Hivyo, ili dhamira ya Tanzania ya kufikia uchumi wa kati itimie, ni muhimu kufikiria namna miji inavyopaswa kukua.
- Katika makala hii, tunatoa mifano ya kitaifa na kimataifa inayoonesha mchango mkubwa zaidi wa kimaendeleo unaotokana na kukua kwa miji midogo ukilinganisha na kukua kwa miji mikubwa kama Dar es Salaam. Tunafikiri sababu kuu ni ukaribu uliopo kati ya miji midogo na maeneo ya vijijini yenye watu wengi walio maskini.
- Kutokana na vielelezo vilivyotolewa, maoni ya makala hii ni kwamba kukuza na kuweka kwenye miji midogo kunaweza kuleta maendeleo na kuondoa umaskini kwa Watanzania wengi zaidi.
- Ni wazi kuwa msukumo wa kufikia uchumi wa kati hautafanikiwa kama tukijikita kwenye kuchochea maendeleo kwenye miji mikubwa tu. Sera zinazoendeleza miji midogo ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo kwa watanzania wote.

## Utangulizi

Mwaka 2007 ilikuwa mara ya kwanza katika historia, dunia kuwa na watu wengi zaidi waishio mijini. Idadi ya watu wanaoishi mijini imekua kwa kasi zaidi miaka ya karibuni. Wakati iliichukuwa Ulaya miaka 110 (1800-1910) kupata ongezeko la wakazi waishio mijini kutoka asilimia 15 hadi 40, Asia na Afrika zimefanya hivyo ndani ya miaka 50 tu (1960-2010). Hii ni kasi mara mbili zaidi ya ile ya Ulaya miaka hiyo. Mara nyingi wataalamu na watunga sera wanafanya tathmini iliyojikita kwenye tofauti zilizomo mijini na vijijini. Ni mara chache sana kuona tathmini hizi zikizingatia utofauti kwenye ukubwa wa miji. Matokeo ya utafiti wetu, yanatushawishi kuwa inabidi kuweka uzito sawa kati ya kutathmini jinsi miji inavyokua na kutambua kwamba miji inakuwa kwa ujumla.


## Utengenezaji wa miji Tanzania

Chukulia mfano wa Dar es Salaam hapa Tanzania. Kutokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, karibia asilimia 10 ya watu wote Tanzania waliishi Dar es Salaam ambao ni takribani watu milioni 4.5. Hii ilikuwa ni idadi kubwa zaidi ya mkusanyiko wa watu wanaoishi mijini Tanzania. Idadi ya watu kwenye jiji la Dar es Salaam imeongezeka kwa kasi ndani ya miaka hamsini iliyopita na ukuaji huu ulisababishwa na uhamiaji wa ndani ya nchi.

Mtazamo huu, unaelekeza kusisitiza uwekezaji wa ndani kwenye miji mikubwa. Na kwa vile wahamiaji hawa wanatoka kwenye maeneo maskini ya vijijini, kuna hoja ya kwamba kuwekeza kwenye majiji pia hushughulikia suala la umaskini. Kielelezo namba 1 kinaonesha kwamba mwaka wa 2012, Dar es Salaam ilikuwa na moja ya tatu ya idadi ya watu waishio mijini. Lakini pia ilikuwa na mgao huo huo mwaka 2002, 1988, 1978 na kurudi nyuma.  Hii inamaanisha kwamba, katika historia ya Tanzania, sehemu nyingine za mijini nje ya Dar es Salaam zilikua kwa kasi sawia na jiji la Dar es Salaam.

Tukiendelea kuigawanya miji midogo katika miji mikuu ya mikoa (yenye wastani wa watu karibia 200,000) na miji mingine midogo (yenye wastani wa watu karibia 20,000), tunaona kwamba kiujumla miji hii midogo ni sehemu kubwa ya watu wanaoishi mijini nchini Tanzania. Kwa hakika, Dar es Salaam siyo mji pekee unaokua. Miji midogo inakua pia na inazidi kuchukua nafasi muhimu. Uhamaji wa watu kutoka vijijini kwenda mijini ni jambo lisilopingika. Lakini, tusisahau kuwa kuna idadi kubwa ya watu wanaohama kutoka vijijini kwenda kwenye miji midogo – siyo kwenda Dar es Salaam pekee.

## Kielezo namba 1: mgawanyiko ya watu wanoishi mjini




## Kuna umuhimu gani kufikiria jinsi miji inavyokua?

Athari za ukuaji wa miji kwenye uchumi na kupunguza umaskini zinategemea mambo matatu yanayohusiana: (i) mkusanyiko wa watu na biashara, na gharama zinazohusiana na msongamano (ii) uhusiano wa kiuchumi kati ya miji na vijiji na (iii) mtiririko wa watu wanaohama kutoka vijijini kwenda mijini.

Kwa mfano, watalaamu wanaamini kuwa mkusanyiko wa watu unaweza kuboresha uchumi kwa sababu ya ongezeko katika ufanisi na fursa zinazojitokeza panapo mkusanyiko mkubwa wa watu. Hata hivyo, miji ikiwa na watu wengi sana, faida za kuishi mjini huanza kutoweka na gharama za kuhimili msongamano zinaweza kusababisha kuporomoka kwa uchumi.

Pia, kuna mchango chanya wa miji inayopanuka katika vijiji au maeneo jirani kupitia ongezeko la biashara, utumaji wa fedha kutoka mijini kama misaada na zawadi, ongezeko katika kipato cha wakulima, na uzalishaji wa kazi zisizokuwa za kilimo vijijini. Kiujumla, ni vigumu kusema kama faida ni nyingi zaidi watu wakiishi kwenye miji mikubwa michache au pale wanaposambaa kwenye miji mingi midogo midogo.

Watu wengi walio maskini huishi vijijini na mara nyingi hua si rahisi kwao kuhama kwa sababu ya vikwazo mbali mbali. Inawezekana kwamba ni rahisi zaidi kwao kuhamia na kukamata fursa za kazi zinazopatikana kwenye miji midogo iliyowakaribia kuliko kwenye miji mikubwa iliyo mbali.

## Uzoefu wa kimataifa.

Njia moja ya kujifunza zaidi juu ya michango ya miji midogo na ajira zisizo za kilimo vijijini ni kuangalia uzoefu wa kimataifa. Tuchukue mfano wa nchi mbili zinazokua kiuchumi kwa kasi sawa, lakini kwenye nchi ya kwanza watu wanahamia kwenye miji mikubwa na kwenye nchi ya pili wanahamia kwenye miji midogo. Je, nchi ipi itapunguza umaskini kwa kasi kubwa zaidi? Tathmini ya nchi 51 duniani kati ya mwaka 1980 na 2004 inatuonesha kwamba kuhamia kwenye miji midogo inasaidia kupunguza umaskini kwa kasi zaidi.

## Uzoefu kutoka Tanzania

Ili kufanya tathmini kama hii ya kimataifa katika nchi ya Tanzania, tunahitaji takwimu ambazo ni wakilishi kwa nchi nzima na zilizokusanywa kwa kipindi kirefu ili kuweza kutambua kikamilifu faida au hasara za uhamiaji. Ili kufanikisha zoezi hili, ni vizuri kuwa na takwimu za wahamiaji kabla ya kuhama na miaka kumi au ishirini baada ya kuhama ili kupata takwimu zinazoonesha maisha halisia ya wahamiaji baada ya kujishikiza vizuri kule walikohamia.


Takwimu hizi hazipo kitaifa, lakini zipo kwa mkoa wa Kagera na tunaweza kujifunza kutokana nazo. Tuna takwimu wakilishi za watu 4,323 waliokua wakiishi mkoani Kagera 1991-94. Mwaka 2010, watu hawa walisailiwa kwa mara nyingine ili kupima maendeleo yao ya kiuchumi katika kipindi cha miongo miwili na kulinganisha kati ya wale waliobaki na wale waliohama.

Watu hawa wa Kagera walipata maendeleo makubwa ya kiuchumi katika kipindi hiki cha miaka 18. Lakini maendeleo hayo yalitofautiana kutokana na: (i) kama mtu alihamia sekta nyingine kutoka kwenye sekta ya kilimo (ii) kama mtu alihamisha makazi kutoka vijiji na (iii) kama alihama, alihamia wapi.

Kwanza, takwimu za Kagera zinaonesha kuwa kwa wastani, kipato cha kundi la watu waliohamia miji mikubwa kilikua karibu mara sita ya kipato cha wale waliobaki kijijini kwenye sekta ya kilimo na mara mbili zaidi ya wale waliohamia miji midogo (kielelezo namba 2).


Kwa kutumia vigezo vya kimataifa, Dar es Salaam na Mwanza ndiyo miji pekee Tanzania, kwa sababu ina wakazi wasiopungua 500,000. Lakini matokeo ya utafiti huu hayabadiliki tukichukua Dar es Salaam kuwa jiji pekee au tukiongeza orodha na kujumuisha miji yote ambayo imepewa hadhi ya kuwa “jiji” na serikali ya Tanzania.

## Kielezo namba 2: Ukuaji wa kiuchumi baada ya miaka 18





Pili, mchanganuo wa watu waliohama na sehemu walizohamia unaonesha kuwa asilimia kubwa ya watu waliohama kwenye vijiji walihamia kwenye miji midogo na sio kwenye miji mikubwa licha ya kuwapo kwa ongezeko kubwa la kipato linaloambatana na kuhamia kwenye miji mikubwa (kielelezo namba 3).

## Kielezo namba 3: mgawanyiko wa watu 2010




Tatu, tukiangalia gawio la ukuaji kiuchumi kwa ujumla, tunaona kuwa asilimia 41 ya ukuaji wa kiuchumi ulioonekana katika kipindi hiki cha miaka 18 ulichangiwa na watu waliohamia kwenye miji midogo ukilinganisha na asilimia 20 uliochangiwa na watu waliohamia miji mikubwa (kielelezo namba 4). Hivyo, msukumo wa kuhamia kwenye miji midogo unachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa jumla wa kiuchumi zaidi ya msukumo wa kuhamia kwenye miji mikubwa.

## Kielezo namba 4: Gawio katika jumla ya ukuaji




Nne, kielelezo cha 4 kimeonesha kuwa mchango wa miji midogo katika kuleta maendeleo ni mkubwa (mara 2 ya mchango wa miji mikubwa). Katika kupunguza umaskini, mchango wa miji midogo ni mkubwa zaidi (karibu mara 3 ya mchango wa miji mikubwa) kama kielelezo cha 5 kinavyoonesha.

## Kielezo namba 5: Gawio katika jumla ya upunguzaji umaskini




Takwimu hizi zinatuonesha kuwa watu wengi wanaohama vijijini wanahamia kwenye miji midogo na ni hao hao wanaochangia zaidi maendeleo na kupunguza umaskini. Bila shaka, nafasi ya miji midogo katika kuchangia maendeleo ni kubwa.

Matokeo hayo yanaonesha kwamba, licha ya mafanikio makubwa ya kiuchumi yapatikanayo kwa kuhamia kwenye miji mikubwa, watu wachache wanahamia huko. Na licha ya ongezeko dogo la kipato kwa wastani linaloambatana na kuhamia kwenye miji midogo,watu wengi wanahamia huko. Hivyo, katika miji midogo, maendeleo yanaongezeka kiasi lakini kwa watu wengi.

Ili kuelewa kwa nini watu wengi wanahamia kwenye miji modogo, lazima tuelewe vigezo vinavyotumika (hasahasa na watu masikini) kuchagua pahala pa kuhamia. Tunashawishika kuwa licha ya kipato kidogo na maendeleo ya wastani, watu maskini bado wanavutiwa zaidi kuhamia kwenye miji midogo kwa sababu ya ukaribu na nyumbani, mtandao mkubwa wa watu walionao, utofauti mdogo kitamaduni na mambo mengine kama hayo.

## Miji midogo kama nyenzo ya kukuza uchumi.

Mtazamo huu wa muundo na ukuaji wa miji unaibua maswali kadhaa juu ya chanzo cha maendeleo na kupunguza umasikini. Pia unaibua maswali magumu ya kisera. Je, Serikali ya Tanzania iegemee kwenye sera na uwekezaji wa umma unaopendelea miji midogo kuliko ule unaopendelea miji mikubwa?

Kuongeza uelewa wetu juu ya mambo wanayozingata watu wakati wa kuchagua pahala pa kuhamia, kunaweza kusaidia kufafanua faida za kuendeleza miundombinu (umeme, barabara, mawasiliano, afya, elimu) katika kuvutia wahamiaji kutoka vijijini kwenda kwenye miji midogo na kuhakikisha watu wenye ujuzi mkubwa wa kikazi pia wanavutiwa kubaki

kwenye miji hiyo.

Ni vizuri kulifikiria swali hili kwenye muktadha wa dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025, unaoainisha matamanio ya nchi kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025 kwa kubadilisha mfumo wa sekta zinazojenga uchumi. Kwa nchi ya Tanzania, matokeo ya utafiti wetu yanaunga mkono kwa nguvu zote mfumo wa viwanda uliojikita kwenye mali asili. Yaani, mfumo utakaosaidia viwanda vya kusindika mazao na viwanda vingine vinavyoongeza thamani ya bidhaa kujengwa katika miji midogo, jirani na wazalishaji vijijini. Huu ni mwanya mzuri wa kuleta maendeleo kwa wote huku watu maskini wakinufaika kupitia uhamiaji na ukaribu kati ya miji hii midogo na vijiji.

Kuwavutia watu wenye ujuzi mkubwa kikazi kuishi kwenye miji midogo ni muhimu ili kuweza kuvuna zaidi faida zitokanazo na mikusanyiko ya watu na uwepo wa watu wenye uwezo tofauti wa kikazi, bila kuingia gharama za kupambana na msongamano wa watu. Zaidi ya miundombinu, mambo mengine yatakayosaidia kuendeleza miji midogo ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa nyumba za kuishi, sera endelevu za ardhi, sera zitakazowavutia watu wenye ujuzi na makampuni, mafunzo ya ujasiriamali kwenye miji midogo na kuweka juhudi katika kuhakikisha ongezeko la thamani katika bidhaa zilizopo eneo husika.

Je, Tanzania inaweza kuwa nchi ya uchumi wa kati bila kila sehemu ya nchi hii kufuzu kuingia kwenye kipato cha kati? Je, msukumo wa kufikia uchumi wa kati utafanikiwa kama tukijikita kwenye kusukuma maendeleo kwenye miji mikubwa tu? Ni wazi kuwa majibu ya maswali haya mawili ni hapana. Hivyo, kufikiria kwa umakini maendeleo ya miji midogo ni nyenzo muhimu katika kutunga sera zitakazoleta maendeleo kwa watanzania wote.

Makala hii iliandaliwa Septemba 2015 kwa maombi ya Tume ya Mipango ya Ofisi ya Rais Tanzania, ili kuchangia katika maandalizi ya Mpango wa pili wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2016/2017 – 2020/2021). Iliandikwa kama sehemu ya mradi wa IGC "urbanization and poverty reduction: the role of secondary towns". Tunawashukuru Pantaleo Kessy, Mujobu Moyo, Benno Ndulu na Johnson Nyela kwa maoni yao muhimu. Matokeo ya utafiti, tafsiri, na hitimisho kwenye makala hii ni ya waandishi.Maoni haya yanaweza yasiwakilishe mtizamo wa Benki ya Dunia na mashirika yake tanzu au Wakurugenzi watendaji wa Benki ya Dunia au serikali wanazoziwakilisha. Tafasiri kwa Kiswahili imefanywa na Privatus Karugendo na Mujobu Moyo. Makala hii inapatikana kwenye mtandao kwa kutembelea http://www.theigc.org/publication/urbanisation-and-poverty-reduction-swahili/. Takwimu na maelezo zaidi kwa lugha ya Kiingereza zinapatikana kwa kutembelea http://www.theigc.org/publication/secondary-towns-and-poverty-reduction-in-tanzania/